TANGAZO LA SERIKALI Na 809 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MJI WA NYEHUNGE YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Mji wa Nyehunge ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Eneo la Upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa eneo

3. Mipango ya jumla na ya kina kwenye eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa.

________

JEDWALI

________

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

’Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK1 yenye majira - nukta 420775.998MS, 9721952.443KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS120$^0$MS kwa umbali wa kilomita 1.8 kwa kukatisha barabara iendayo Kahunda hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK2 yenye majira - nukta 422635.087MS, 9722072426KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS130$^0$MS kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK3 yenye majira - nukta 423086.390MS, 9721608.029KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS149$^0$MS kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK4 yenye majira - nukta 423227.871MS, 9721002.126KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS113$^0$MG kwa umbali wa kilomita 0.9 kwa kukatisha barabara iendayo Sengerema hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK5 yenye majira - nukta 422438.378MS, 9720435.708KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS234$^0$KS hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK6 yenye majira - nukta 422437.972MS, 9719589.453KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG97$^0$MG kwa umbali wa kilomita 1.4 kwa kukatisha barabara itokayo Kayenze hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK7 yenye majira - nukta 421043.800MS, 9719503.595KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ126$^0$MG kwa umbali wa kilomita 0.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK8 yenye majira - nukta 420479.056MS, 9720266.583KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ142$^0$KZ kwa umbali wa kilomita 1.1 kwa kukatisha barabara itokayo Geita hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK9 yenye majira - nukta 420502.216MS, 9721386.848KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ155$^0$MS kwa umbali wa kilomita 0.6 ulipoanzia.

Dodoma,
19 Oktoba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*